# MUHTASARI WA PATO LA TAIFA ROBO YA TATU (JULAI – SEPTEMBA) 2023, BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015

Wizara ya Fedha
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Januari 2024

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ..... ii
Orodha ya Vielelezo ..... iii
Orodha ya Viambatisho ..... iv
1.0 Utangulizi ..... 2
1.1 Uchumi wa Dunia ..... 2
1.2 Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 2
1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ..... 2
1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ..... 3
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania ..... 4
1.5.1 Pato la Taifa Robo ya Tatu Mwaka 2023 ..... 5
1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Tatu Mwaka 2023 ..... 5
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Robo ya Tatu Mwaka 2023 ..... 6
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Tatu Mwaka 2023 ..... 7
2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi ..... 7
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi ..... 7
2.1.1 Mazao ..... 7
2.1.2 Mifugo ..... 8
2.1.3 Misitu ..... 8
2.1.4 Uvuvi ..... 9
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe ..... 9
2.3 Uzalishaji Viwandani ..... 10
2.4 Umeme ..... 10
2.5 Usambazaji Maji ..... 10
2.6 Ujenzi ..... 11
2.7 Biashara na Matengenezo ..... 12
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo ..... 12
2.9 Malazi na Huduma za Chakula ..... 12
2.10 Habari na Mawasiliano ..... 13
2.11 Fedha na Bima ..... 13
2.12 Upangishaji Majengo ..... 14
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi ..... 14
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala ..... 15
2.15 Utawala na Ulinzi ..... 15
2.16 Elimu ..... 15
2.17 Afya na Huduma za Jamiii ..... 16
2.18 Huduma Nyingine za Jamii ..... 16
3.0 Hitimisho ..... 16

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Tatu Mwaka 2019 - 2023 ....................................... 10
Jedwali Na. 2: Viashiria vya Shughuli za Habari na Mawasiliano Mwaka 2019 - 2023................. 13

# Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Tatu, Mwaka 2022 na 2023 ........ 3
Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Tatu ya Mwaka 2019 – 2023 ........ 4
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023 ........ 5
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika ........ 6
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Tatu Mwaka 2023 ........ 6
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo yaTatu, Mwaka 2022 na 2023 ........ 8
Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023 ........ 11
Kielelezo Na. 8: Thamani ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023 ........ 14

## Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 - Sh. Milioni ........................................................................................................................ 18
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Asilimia ........................................................................................................................ 20
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni ........................................................................................ 22
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Asilimia ........................................................................... 24

## 1.0 Utangulizi

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina za mwenendo wa shughuli za uchumi. Kiashiria hiki hutumika katika kutathmini mwenendo wa shughuli za kiuchumi kwa vipindi vifupi vifupi kwa lengo la kutunga na kutathmini sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika nchi.

## 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya mwezi Oktoba 2023, uchumi wa dunia ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 3.0 mwaka 2023 sawa na kiwango kilichokadiriwa kwenye Maoteo yaliyofanyika mwezi Julai Mwaka 2023.

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo: kuimarika kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa, na kuendelea kupungua kwa gharama za usafirishaji. Aidha, uchumi wa dunia umeonesha kuimarika zaidi pamoja na mfumuko wa bei kukadiriwa kupungua na kufikia asilimia 6.8 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2023 kutoka asilimia 8.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha ambazo zimechangia kufanya bei za bidhaa kimataifa kuwa imara.

## 1.2 Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mjibu wa ripoti ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya mwezi Oktoba 2023, ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara ulikadiriwa kuongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.3. Kiwango hicho ni sawa na upungufu kwa asilimia za pointi 0.2 ikilinganishwa na makadirio yaliyofanyika kwenye maoteo ya mwezi Julai 2023. Uchumi wa nchi ya Afrika Kusini ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 0.9 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia za pointi 0.6 kutoka kadirio la ukuaji wa asilimia 0.3 lililokuwa limekadiriwa kwenye ripoti ya Julai 2023. Aidha, katika kipindi hicho kasi ya ukuaji wa uchumi wa Nigeria ilikadiriwa kupungua hadi asilimia 2.9 ikilinganishwa na maoteo ya mwezi Julai 2023 ya ukuaji wa asilimia 3.5.


## 1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa ripoti ya makadirio ya ukuaji wa uchumi ya mwezi Oktoba 2023 inayotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ukuaji wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.3 mwaka

2023 ikiwa ni pungufu kwa pointi za asilimia 0.2 ikilinganishwa na asilimia 3.5 ya maoteo ya mwezi Julai 2023.

Tathmini ya ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika inaonesha kuwa uchumi wa nchi ya Afrika Kusini umepungua kwa kiwango hasi cha asilimia 0.2 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.8 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Namibia ulikua kwa kiwango cha asilimia 7.2 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Botswana ulikua kwa kiwango cha asilimia 0.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.3 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Tatu, Mwaka 2022 na 2023**





**Chanzo**: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2023

## 1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika robo ya tatu ya mwaka 2023 zilizopatikana kwenye tovuti za taasisi hizo zimeonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji chanya wa uchumi. Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Rwanda ilikuwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na asilimia 10.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango cha asilimia 5.3 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ukilinganishwa na asilimia 5.2 katika robo ya tatu mwaka 2022. Taarifa za mwenendo

wa ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2023 bado hazijawekwa kwenye tovuti za nchi husika.

**Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Tatu ya Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo**: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi husika, 2023

## 1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania


Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa robo ya tatu (Julai - Septemba) 2023 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *System of National Accounts 2008 (2008 SNA)*. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na bei za mwaka 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka. Kutokana na mapitio ya Sera hii na maboresho yaliyofanyika kwenye takwimu za urari wa biashara zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, takwimu za Pato la Taifa za mwaka 2017 - 2022 zimefanyiwa mapitio.

### 1.5.1 Pato la Taifa Robo ya Tatu Mwaka 2023

Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika (*current prices*) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 45.8 kutoka Shilingi trilioni 40.1 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 (*constant prices*) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 35.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 kutoka Shilingi trilioni 33.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni sawa na ongezeko halisi la asilimia 5.3.

**Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023**





**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

### 1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Tatu Mwaka 2023

Mchanganuo wa mchango wa makundi makuu ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika robo ya tatu ya mwaka 2023 unaonesha kuwa shughuli za huduma zilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 42.5, zikifuatiwa na shughuli za msingi asilimia 32.7, na shughuli za kati asilimia 24.8. Mchango wa makundi makuu ya shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kwa bei za mwaka husika kabla ya kujumuisha kodi.

**Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika**





**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu 2023

### 1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Robo ya Tatu Mwaka 2023

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2023, shughuli ya kiuchumi ya Fedha na Bima iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 18.7, ikifuatiwa na Habari na Mawasiliano (asilimia 11.3), Uchimbaji wa Madini na Mawe (asilimia 10.2), Umeme (asilimia 9.7), Huduma Nyingine za Jamii zinazojumuisha Sanaa na Burudani na Shughuli za Kaya katika Kuajiri (asilimia 9.0), na Huduma za Chakula na Malazi (asilimia 7.4).

**Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Tatu Mwaka 2023**




**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

### 1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Tatu Mwaka 2023

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 zilichangia katika ukuaji wa uchumi kwa viwango tofauti. Katika kipindi hicho, zilizochangia zaidi katika ukuaji zilikuwa ni pamoja na: Kilimo ambacho kilichangia kwenye ukuaji kwa asilimia 14.2, ikifuatiwa na Fedha na Bima (asilimia 13.0), Uchimbaji wa Madini na Mawe (asilimia 10.4), Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 9.1), Ujenzi (asilimia 7.6), na Uzalishaji Viwandani (asilimia 7.3).

## 2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi

### 2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama. Shughuli hizi zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

### 2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora pamoja kuimarika kwa huduma za ugani.

**Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo yaTatu, Mwaka 2022 na 2023**




**Chanzo:** Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

Mazao ambayo yalichangia zaidi katika ukuaji wa shughuli ya mazao katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ni pamoja na mahindi yaliyoongezeka kwa asilimia 10.8 kutoka tani elfu 712 mwaka 2022 hadi tani elfu 789 mwaka 2023, Mpunga uliongezeka kwa asilimia 6.2 kutoka tani elfu 339 mwaka 2022 hadi tani elfu 360 mwaka 2023, mihogo iliongozeka kwa asilimia 3.9 kutoka tani elfu 304 mwaka 2022 hadi tani elfu 316 mwaka 2023. Ndizi ziliongezeka kwa asilimia 15.1 kutoka tani elfu 146 mwaka 2022 hadi tani elfu 168 mwaka 2023. Vile vile uzalishaji wa Mtama/Ulezi uliongezeka kwa asilimia 16.0 kutoka tani elfu 19 mwaka 2022 hadi tani elfu 22 mwaka 2023.

### 2.1.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.1 ambacho ni sawa na kiwango cha ukuaji cha kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia lishe bora kutokana na mazao ya Mifugo.

### 2.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu ambayo ni Pamoja na: magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu na juhudi za Serikali katika kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

### 2.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uvuvi ilitokana na juhudi za Serikali katika kusimamia uvunaji wa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

## 2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (mfano petroli) au gesi (mfano gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji kutoka juu ya ardhi au kwenye visima. Uchimbaji wa madini na mawe pia unajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

i. Madini ya makaa ya mawe;
ii. Petroli na gesi asilia;
iii. Uchimbaji wa madini ya chuma; na
iv. Madini ya kokoto na mawe.

Katika robo ya tatu ya Mwaka 2023, shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 10.2 ikilinganishwa na asilimia 9.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa makaa ya mawe, gesi asilia, chumvi, fedha na pozzolana ambayo hutumika kutengeneza saruji.

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Tatu Mwaka 2019 - 2023**

| Madini | Kipimo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fedha | Tani | 2,626 | 3,095 | 3,702 | 3,519 | 3,589 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 131,705 | 196,502 | 191,607 | 441,407 | 918,255 |
| Chumvi | Tani | 22,027 | 20,858 | 26,556 | 73,566 | 52,935 |
| Gesi asilia | Mscf | 16,836 | 14,029 | 15,775 | 19,866 | 21,996 |

**Chanzo:** Wizara ya Madini, 2023

## 2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazochakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka kwa asilimia 4.2 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

## 2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia kwenye miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme unatokana na vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa nishati ya umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozalishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali. Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za umeme kilikuwa asilimia 9.7 ambacho ni sawa na ukuaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha umeme kilichosambazwa kiliongezeka hadi saa za kilowati milioni 2,175 mwaka 2023 kutoka saa za kilowati milioni 1,983 kipindi kama hicho mwaka 2022.

## 2.5 Usambazaji Maji


Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na

kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 99.1 kutoka mita za ujazo milioni 97.3 zilizozalishwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kilikuwa asilimia 1.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 0.1 kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, 2023

## 2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli za ujenzi zinajumuisha, ujenzi wa nyumba za kuishi na nyumba za makazi, ujenzi wa majengo ya biashara au ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Shughuli hii  pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.5 ikilinganishwa na asilimia 5.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika ujenzi. Bidhaa za ndani zilizochangia ukuaji wa shughuli hii ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji saruji na bidhaa za chuma.

## 2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Shughulki hii pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa binafsi za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli ya biashara na matengenezo iliongezeka hadi asilimia 3.0 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 kutoka asilimia 2.2 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa zilizozalishwa viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

## 2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo iliongezeka kwa asilimia 5.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 7.3 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara katika kipindi hicho.

## 2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya malazi na huduma za chakula iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 13.2 kipindi kama hicho

mwaka 2022. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya malazi na huduma za chakula katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ilichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini ambao waliongezeka hadi watalii 540,667 kutoka watalii 459,016 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2022.

## 2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kama vile utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari ikiwa ni pamoja na uchakataji wa taarifa.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya habari na mawasiliano kiliongezeka hadi asilimia 11.3 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 kutoka asilimia 10.8 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa maongezi ya simu kwa dakika, huduma ya utumaji ujumbe mfupi na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

**Jedwali Na. 2: Viashiria vya Shughuli za Habari na Mawasiliano Mwaka 2019 - 2023**

| Kiashiria cha Robo ya Tatu | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maongezi ya sauti kwa dakika (Milioni) | 18,207 | 21,966 | 25,203 | 33,374 | 39,070 |
| Idadi ya ujumbe mfupi Ndani na Nje ya Nchi (Milioni) | 24,573 | 31,758 | 35,605 | 40,211 | 49,066 |
| Watumiaji wa huduma za kifedha (Wastani) ('000’) | 23,693 | 30,587 | 33,155 | 39,591 | 51,369 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 2023


## 2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma ya fedha na bima iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 18.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 kutoka asilimia 8.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli ya fedha na bima ulichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 24.8 kwa amana za wateja kutoka shilingi trilioni 27.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 34.6 robo ya tatu ya mwaka 2023; kuongezeka kwa asilimia 22.3

kwa mikopo kutoka shilingi trilioni 25.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 31.1 katika robo ya tatu ya mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 8: Thamani ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Tatu Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania, 2023

## 2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya upangishaji majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.2 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

## 2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli za kitaalam, kisanyansi na kiufundi iliongezeka kwa asilimia 4.1 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

## 2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala kiliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.6 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

## 2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya utawala na ulinzi iliongezeka kwa asilimia 5.1 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilima 6.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za Serikali katika mishahara, kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

## 2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.1 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za utoaji wa elimu za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mishahara na matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

### 2.17 Afya na Huduma za Jamiii

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utoaji wa huduma za afya iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 7.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma katika vituo vya umma na binafsi na kuongezeka kwa ya mishahara ya watumishi wa umma.

### 2.18 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya huduma nyingine za jamii iliongezeka kwa asilimia 9.0 katika robo ya tatu ya mwaka 2023 kiwango sawa kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuendelea kuongezeka kwa watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii kulichangia ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

## 3.0 Hitimisho

Katika robo ya tatu ya mwaka 2023, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.3 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, shughuli zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa asilimia 5.3 ni

pamoja na: kilimo asilimia 14.2, fedha na bima (asilimia 13.0), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 10.4), usafirishaji na uchukuzi (asilimia 9.1), ujenzi (asilimia 7.6) na uzalishaji viwandani (asilimia 7.3).

**Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 - Sh. Milioni**

| Mwaka | Robo | Kilimo | Madini na Mawe | Viwanda | Umeme | Maji safi na maji taka | Ujenzi | Biashara na matengenezo | Malazi na huduma ya chakula | Uchukuzi na uhifadhi mizigo | Habari na mawasiliano | Fedha na bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | | 23,952,077 | 3,687,273 | 6,919,794 | 815,297 | 381,760 | 9,253,082 | 8,444,243 | 1,397,782 | 6,577,706 | 1,560,064 | 3,764,113 |
| 2015 | | 25,234,560 | 4,055,619 | 7,411,672 | 798,801 | 390,758 | 10,446,797 | 8,747,862 | 1,421,916 | 6,929,895 | 1,681,098 | 4,189,021 |
| 2016 | | 26,436,338 | 4,356,709 | 8,213,364 | 869,262 | 417,899 | 11,960,720 | 9,260,703 | 1,480,052 | 7,324,856 | 1,718,548 | 4,235,515 |
| 2017 | | 27,999,284 | 4,588,624 | 8,889,818 | 877,667 | 444,660 | 13,765,005 | 9,820,627 | 1,525,619 | 7,815,845 | 1,824,472 | 4,115,393 |
| 2018 | | 29,504,236 | 4,659,195 | 9,623,501 | 928,174 | 477,510 | 15,655,747 | 10,434,333 | 1,604,391 | 8,736,561 | 1,989,717 | 4,094,972 |
| 2019 | | 30,802,622 | 5,485,112 | 10,184,558 | 994,879 | 510,411 | 17,802,021 | 10,961,777 | 1,645,950 | 9,493,191 | 2,133,312 | 4,281,167 |
| 2020 | | 32,323,673 | 5,887,452 | 10,646,279 | 1,049,610 | 540,159 | 19,421,672 | 11,197,266 | 1,419,654 | 10,293,276 | 2,313,032 | 4,412,967 |
| 2021 | | 33,588,777 | 6,442,881 | 11,155,762 | 1,154,204 | 575,213 | 20,249,939 | 11,623,456 | 1,514,711 | 10,658,344 | 2,524,610 | 4,599,677 |
| 2022 | | 34,711,277 | 7,146,141 | 11,624,144 | 1,242,132 | 606,754 | 21,131,032 | 12,046,448 | 1,651,099 | 11,061,950 | 2,712,411 | 5,024,141 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | 1 | 6,335,448 | 937,448 | 1,621,405 | 201,849 | 87,893 | 2,182,230 | 2,054,479 | 346,623 | 1,625,429 | 342,909 | 912,095 |
| | 2 | 5,877,120 | 871,899 | 1,706,772 | 182,845 | 94,708 | 2,507,336 | 2,073,942 | 339,327 | 1,616,710 | 380,305 | 927,895 |
| | 3 | 4,450,294 | 929,381 | 1,788,128 | 213,998 | 97,099 | 2,228,708 | 2,035,245 | 361,470 | 1,686,150 | 414,058 | 960,721 |
| | 4 | 7,289,215 | 948,546 | 1,803,489 | 216,605 | 102,059 | 2,334,808 | 2,280,578 | 350,362 | 1,649,417 | 422,793 | 963,401 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | 1 | 6,605,887 | 923,326 | 1,733,636 | 211,828 | 96,862 | 2,438,046 | 2,093,973 | 346,778 | 1,654,599 | 386,446 | 995,846 |
| | 2 | 6,347,239 | 965,335 | 1,820,111 | 199,281 | 92,862 | 2,690,105 | 2,195,254 | 345,054 | 1,676,064 | 412,841 | 1,011,653 |
| | 3 | 4,656,388 | 960,427 | 1,939,664 | 192,215 | 99,585 | 2,601,253 | 2,162,776 | 372,080 | 1,764,202 | 441,478 | 1,076,143 |
| | 4 | 7,625,045 | 1,206,532 | 1,918,260 | 195,477 | 101,448 | 2,717,393 | 2,295,860 | 358,003 | 1,835,030 | 440,334 | 1,105,380 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2016 | 1 | 6,788,342 | 1,017,609 | 1,965,656 | 214,850 | 95,779 | 2,859,933 | 2,295,506 | 358,142 | 1,818,390 | 401,047 | 1,111,056 |
| | 2 | 6,853,095 | 1,109,064 | 1,996,019 | 210,034 | 100,816 | 2,995,869 | 2,318,553 | 347,167 | 1,819,827 | 421,552 | 1,052,954 |
| | 3 | 4,936,684 | 1,098,979 | 2,080,908 | 214,673 | 103,584 | 3,208,669 | 2,300,383 | 385,323 | 1,854,653 | 451,160 | 1,053,955 |
| | 4 | 7,858,218 | 1,131,055 | 2,170,783 | 229,706 | 117,720 | 2,896,249 | 2,346,262 | 389,420 | 1,831,986 | 444,789 | 1,017,550 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2017 | 1 | 7,232,687 | 1,118,373 | 2,067,899 | 223,828 | 97,295 | 3,204,078 | 2,338,462 | 374,854 | 1,914,669 | 451,535 | 1,046,337 |
| | 2 | 7,283,393 | 1,057,691 | 2,187,504 | 207,472 | 105,045 | 3,631,267 | 2,437,206 | 359,355 | 1,910,951 | 448,743 | 1,028,316 |
| | 3 | 5,137,220 | 1,144,597 | 2,365,766 | 222,983 | 113,969 | 3,198,026 | 2,434,184 | 395,146 | 1,982,315 | 459,599 | 998,080 |
| | 4 | 8,345,985 | 1,267,964 | 2,268,650 | 223,383 | 128,352 | 3,731,635 | 2,610,775 | 396,263 | 2,007,909 | 464,595 | 1,042,660 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2018 | 1 | 7,717,887 | 1,054,655 | 2,173,169 | 225,308 | 100,913 | 3,703,467 | 2,441,251 | 391,664 | 2,082,426 | 522,189 | 1,017,425 |
| | 2 | 7,716,454 | 1,129,287 | 2,259,893 | 221,254 | 111,470 | 3,846,566 | 2,532,751 | 383,333 | 2,169,733 | 506,979 | 1,004,583 |
| | 3 | 5,333,853 | 1,166,716 | 2,530,756 | 235,525 | 126,137 | 3,711,275 | 2,614,972 | 425,407 | 2,222,813 | 481,221 | 1,036,203 |
| | 4 | 8,736,041 | 1,308,537 | 2,659,683 | 246,088 | 138,991 | 4,394,440 | 2,845,359 | 403,987 | 2,261,589 | 479,328 | 1,036,760 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2019 | 1 | 8,138,907 | 1,159,804 | 2,280,570 | 249,013 | 108,984 | 4,201,084 | 2,526,618 | 390,255 | 2,312,794 | 563,425 | 1,069,001 |
| | 2 | 8,039,176 | 1,323,857 | 2,384,031 | 239,855 | 118,551 | 4,636,133 | 2,672,669 | 393,345 | 2,322,004 | 538,389 | 1,046,651 |
| | 3 | 5,485,754 | 1,413,025 | 2,749,036 | 247,875 | 139,826 | 4,350,024 | 2,794,020 | 442,538 | 2,407,844 | 516,803 | 1,085,090 |
| | 4 | 9,138,785 | 1,588,425 | 2,770,921 | 258,136 | 143,049 | 4,614,781 | 2,968,470 | 419,812 | 2,450,548 | 514,695 | 1,080,425 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2020 | 1 | 8,470,457 | 1,365,988 | 2,387,165 | 264,424 | 116,821 | 4,408,146 | 2,651,091 | 400,323 | 2,505,607 | 609,865 | 1,116,178 |
| | 2 | 8,368,112 | 1,438,625 | 2,479,030 | 247,857 | 124,044 | 5,203,762 | 2,668,584 | 330,902 | 2,541,456 | 592,089 | 1,079,697 |
| | 3 | 5,837,993 | 1,491,966 | 2,886,991 | 258,781 | 150,811 | 4,955,258 | 2,855,091 | 331,271 | 2,576,818 | 561,022 | 1,105,727 |
| | 4 | 9,647,111 | 1,590,872 | 2,893,092 | 278,547 | 148,483 | 4,854,506 | 3,022,500 | 357,157 | 2,669,394 | 550,056 | 1,111,366 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2021 | 1 | 8,688,965 | 1,489,458 | 2,532,535 | 283,589 | 127,311 | 4,641,094 | 2,768,122 | 374,418 | 2,730,301 | 663,760 | 1,137,283 |
| | 2 | 8,581,277 | 1,574,503 | 2,589,415 | 277,917 | 134,491 | 5,302,015 | 2,793,230 | 364,386 | 2,666,798 | 661,706 | 1,114,001 |
| | 3 | 6,141,413 | 1,677,259 | 2,995,394 | 284,691 | 157,663 | 5,241,139 | 2,915,871 | 378,526 | 2,560,195 | 607,185 | 1,150,525 |
| | 4 | 10,177,121 | 1,701,661 | 3,038,419 | 308,007 | 155,747 | 5,065,691 | 3,146,233 | 397,381 | 2,701,050 | 591,959 | 1,197,867 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2022 | 1 | 9,059,515 | 1,634,049 | 2,692,630 | 307,057 | 142,426 | 4,893,120 | 2,931,300 | 379,909 | 2,765,442 | 703,102 | 1,245,051 |
| | 2 | 8,858,422 | 1,665,101 | 2,711,874 | 302,142 | 147,326 | 5,512,600 | 2,918,632 | 411,599 | 2,775,195 | 704,239 | 1,220,918 |
| | 3 | 6,384,936 | 1,838,926 | 3,127,447 | 312,386 | 157,751 | 5,532,373 | 2,980,729 | 428,373 | 2,746,367 | 672,848 | 1,251,187 |
| | 4 | 10,408,404 | 2,008,066 | 3,092,193 | 320,547 | 159,251 | 5,192,938 | 3,215,788 | 431,217 | 2,774,947 | 632,221 | 1,306,985 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2023 | 1 | 9,384,414 | 1,865,624 | 2,865,062 | 331,948 | 149,709 | 5,151,185 | 3,106,347 | 426,514 | 2,829,232 | 748,368 | 1,416,306 |
| | 2 | 9,074,215 | 1,770,391 | 2,878,496 | 339,510 | 152,141 | 5,637,956 | 3,105,958 | 441,387 | 2,985,541 | 747,707 | 1,411,168 |
| | 3 | 6,640,612 | 2,026,633 | 3,258,720 | 342,642 | 160,561 | 5,668,254 | 3,068,910 | 460,161 | 2,909,290 | 748,551 | 1,485,548 |
| | 4 | | | | | | | | | | | |

**Kiambatisho Na. 1 (Kinaendela.): Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

| Mwaka | Robo | Utawala na Ulinzi | Shughuli za kitaalam, ufundi na sayansi | Huduma zinazohusian na utawala | Upangishaji majengo | Elimu | Afya na huduma za jamii | Huduma nyingine za jamii | Jumla ya Ongezeko la Thamani | Ongeza kodi katika bidhaa | Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | | 4,242,164 | 447,921 | 1,976,260 | 2,828,970 | 2,186,260 | 1,349,941 | 1,088,317 | 80,873,021 | 8,001,090 | 88,874,111 |
| 2015 | | 4,548,604 | 518,123 | 2,183,917 | 2,949,598 | 2,413,306 | 1,419,090 | 1,144,099 | 86,484,736 | 7,864,579 | 94,349,316 |
| 2016 | | 4,793,820 | 606,207 | 2,611,498 | 3,077,086 | 2,665,336 | 1,497,896 | 1,278,046 | 92,803,857 | 8,024,535 | 100,828,393 |
| 2017 | | 4,907,113 | 694,291 | 2,892,463 | 3,211,895 | 2,859,171 | 1,611,999 | 1,409,504 | 99,253,448 | 8,393,240 | 107,646,688 |
| 2018 | | 5,064,968 | 763,332 | 3,054,288 | 3,354,518 | 3,046,789 | 1,746,731 | 1,516,831 | 106,255,796 | 8,924,997 | 115,180,792 |
| 2019 | | 5,238,491 | 821,636 | 3,311,753 | 3,505,485 | 3,257,406 | 1,833,514 | 1,627,511 | 113,890,796 | 9,303,083 | 123,193,879 |
| 2020 | | 5,438,146 | 881,833 | 3,569,800 | 3,663,972 | 3,365,355 | 1,953,479 | 1,668,877 | 120,046,501 | 9,093,315 | 129,139,817 |
| 2021 | | 5,713,411 | 942,013 | 3,817,047 | 3,827,460 | 3,537,611 | 2,065,349 | 1,840,290 | 125,830,755 | 9,647,434 | 135,478,189 |
| 2022 | | 6,024,203 | 996,609 | 3,993,799 | 3,997,460 | 3,724,729 | 2,176,986 | 1,998,754 | 131,870,070 | 10,002,660 | 141,872,730 |
| 2014 | 1 | 1,007,519 | 105,963 | 469,602 | 696,292 | 510,028 | 322,658 | 266,230 | 20,026,099 | 2,102,819 | 22,128,918 |
| | 2 | 1,022,325 | 109,904 | 488,892 | 703,526 | 525,815 | 342,267 | 268,409 | 20,039,997 | 1,866,580 | 21,906,577 |
| | 3 | 1,105,719 | 113,951 | 503,710 | 710,859 | 571,648 | 346,149 | 276,932 | 18,794,219 | 1,989,729 | 20,783,948 |
| | 4 | 1,106,601 | 118,104 | 514,055 | 718,293 | 578,769 | 338,867 | 276,745 | 22,012,706 | 2,041,962 | 24,054,668 |
| 2015 | 1 | 1,033,818 | 122,364 | 519,928 | 725,830 | 557,686 | 331,321 | 277,986 | 21,056,161 | 1,721,421 | 22,777,583 |
| | 2 | 1,067,508 | 126,934 | 532,698 | 733,472 | 573,927 | 344,848 | 279,553 | 21,414,740 | 1,952,108 | 23,366,848 |
| | 3 | 1,227,874 | 131,816 | 552,364 | 741,220 | 640,405 | 377,131 | 291,033 | 20,228,053 | 2,137,973 | 22,366,026 |
| | 4 | 1,219,405 | 137,009 | 578,927 | 749,076 | 641,287 | 365,789 | 295,528 | 23,785,782 | 2,053,077 | 25,838,859 |
| 2016 | 1 | 1,236,354 | 142,513 | 612,386 | 757,042 | 672,749 | 383,295 | 303,604 | 23,034,254 | 1,945,089 | 24,979,343 |
